**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

**SIMU:** 0719102176
0626195174
lucasmalia342@gmail.com

SHULE YA SEKONDARI LUCAS MALIA
S.L.P 51,
RUANGWA.

---

**LMSS/A.1/S.01/001** **04/12/2020**

**MZAZI/MLEZI WA ……………………………………………..………………….**

**YAH: KUCHAGULIWA KWA MWANAO**

**……………………………………………………………………………………**
**KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA LUCAS MALIA.**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **kwanza** katika **Shule ya Sekondari ya Wasichana Lucas Malia** kwa mwaka wa masomo **2020.**

Nampongeza mwanao kwa kuchaguliwa kwake, akumbuke kwamba hii ni bahati kubwa na ya pekee kwake.

**MAHALI SHULE ILIPO;**

**Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Lucas Malia** ipo **Mkoa wa LindiWilaya ya Ruangwa Kata ya Mnacho.** Shule ipo umbali wa kilometa 1 kutoka barabara kuu ya Ruangwa-Nanganga.

Ukifika kijiji cha Chimbila B. Shule ipo upande wa kulia ukitokea Nanganga na ipo kushoto ukitokea Ruangwa.

Aidha shule itafunguliwa mnamo tarehe 06/01/2020 hivyo unasisitizwa kumleta mwanao ili asajiliwe na kuendelea na masomo mapema.

Pamoja na barua hii, pokea,

(a) Fomu ya kupimwa afya yako. Upimwe kwenye Hospitali ya Serikali, hakikisha unapimwa sio kujaziwa fomu tu, na umwelekeze Mganga matatizo ya afya uliyonayo, kwani hatutapokea hoja zozote za ugonjwa kinyume na ripoti ya daktari.
(b) Fomu ya kuonyesha ndugu wa karibu na eneo la shule ikiwa na anuani, namba ya simu na mahali anakoishi pamoja na ahadi ya kutekeleza wajibu. Kwa kumalizia, nakutakia maandalizi mema na safari njema kuja kujiunga nasi.

**KARIBU SANA LUCAS MALIA**

……………………………………….

**GLADNESS H. MAKONGWA**

**Mkuu wa Shule.**

**Mambo muhimu ya kuzingatia**

**1.0 Sare ya shule:**

- Mwanafunzi aje na sketi mbili za bluu anga (light sky blue)
- Sketi zake zisiwe na (belt) mkanda mpana, upana wa belt usizidi sentimeta 05 au inchi moja na nusu pia ziwe na urefu usiozidi sentimita 18 kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la sketi.
- Mshono wa sketi ni linda box moja mbele mashati mawili mapya meupe- tetroni mikono mifupi au Nusu kanzu na Juba kwa wanaovaa Hijab
- Viatu vya ngozi rangi nyeusi vya kamba visivyokuwa na kisigino kirefu jozi mbili.
- Soksi nyeupe jozi mbili kwa ajili ya sare
- Magauni mawili ya rangi ya dark green(kijani kibichi) mshonio wa solo kwa ajili ya kazi za nje yenye mikono mirefu na Juba lake kwa wanaovaa hijab au mikono mifupi kwa wasiovaa (ShambaDress)
- T – Shirt ya kijivu (ya kola) yenye nembo ya shule. (Maelekezo atapewa Shuleni)
- Sweta moja kahawia (Brown)
- Pia mwanafunzi atatakiwa kuwa na kitambulisho cha shule kinachopatikana kwa gharama ya shilingi 3000/=

**1.1 Sare za Michezo**

- Tracksuit rangi ya bluu nyeus(dark blue)
- Raba nyeupe
- Tisheti nyeusi

Mzazi/mlezi na mwanafunzi tafadhali zingatia vipimo hivyo, mwanafunzi atakayeshona na kuja na sketi/shamba dress kinyume na vipimo, rangi na aina ya kitambaa tulichoelekeza hatapokelewa, atarudishwa nyumbai ili aje na sare zilizoelekezwa

- **Mwanafunzi anaweza kushona idadi ya sare kadri ya uwezo wake. Ila inashauriwa awe na angalau sare za darasani mbili na gauni za kazi mbili.**

  Sare ya shule ni kama ilivyoelekezwa katika maelekezo. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare wakati wote wa masomo, na anapokwenda hospitali, mjini au anapokuwa katika shughuli zozote za kishule nje ya eneo la shule. Ni marufuku kabisa kujipamba wakati amevaa sare ya shule akiwa shuleni. Aidha, lipo vazi la kazi za nje ambalo huvaliwa na wanafunzi wanapokuwa katika kazi za mikono nje ya masomo

**2.0 Mahitaji mengine muhimu kwa mwanafunzi**

- Aje na sanduku (nunua sanduku la bati) linalofunga vizuri kwa kuhifadhia nguo na vitu vyake.
- Daftari 10 kubwa (Counter book kuanzia QUIRE 3) na 10 za kawaida
- Mathematical Set (Mkebe)
- Aje na kamusi [Dictionary]
- Godoro 1 jipya la sponji (futi $2\frac{1}{2}$ kwa futi 6)
- Chandarua (Neti) 1 ya rangi ya pink
- Foronya 2 za rangi ya pinki na mto 1
- Shuka mbili za rangi ya pinki
- Ndala za kuogea jozi 1
- Taulo moja
- Mswaki na dawa ya meno
- Chanuo/kitana cha nywele
- Aje na kitenge kipande kimoja pamoja kanga kipande kimoja kwaajili ya kuogea
- Aje na bakuli, sahani, kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula
- Anaweza kuja na pasi ya mkaa kwaajili ya kunyoshea nguo zake
- Pia aje na faili mbili kwaajili ya kuhifadhia nyaraka zake

- Pia aje na Dictionary.
- Aje na rimu mbili ( moja kwa muhula wa kwanza na moja kwa muhula wa pili) rejea kikao cha wazazi kilichofanyika 22 juni 2020 ambacho wazazi walikubaliana kuchangia rimu.

**2.1 Vifaa vya usafi**

- Jembe jipya moja lenye mpini na panga/ fyekeo kwa ajili ya usafi wa mazingira
- Fagio ya chelewa yenye mpini mrefu/fagio ya kawaida
- Ndoo ndogo mbili mpya na kopo la kuogea
- Soft broom moja
- Hard broom moja

Matibabu na mfuko wa afya ya jamii (CHF) 15,000/= (5000/= kwa ajili ya CHF na 10000/= kwa ajili Afya na matibabu) Kwa wenye Bima ya Afya, watachangia Tsh. 10,000/= tu.

**3.0 Chakula**

Mzazi/mlezi unatakiwa kugharamia chakula na mahitaji mengine kwa mwaka kama ifuatavyo;

| S/N | MAHITAJI | GHARAMA ZAKE |
|---|---|---|
| 01 | CHAKULA | 600,000 |
| 02 | MPISHI | 10,000 |
| 03 | MATIBABU NA CHF | 15,000 |
| 04 | MATRON | 10,000 |
| 06 | MLINZI | 10,000 |
| 07 | KUNI | 20,000 |
| 08 | MAJI | 2000 |
| 09 | UMEME | 5000 |
| | **JUMLA KUU** | **672,000/=** |

**NB:** Gharama hizi zitalipwa awamu nne kwa mchanganuo ufuatao;

- Awamu ya Kwanza inaanza 11/01/2021-26/03/2021= Tshs. 250,000/= (laki mbili, na elfu hamsini tu).
- Awamu ya Pili kuanzia 12/04/2021-04/06/2021 =Tshs 160,000(laki moja na elfu sitini tu)
- Awamu ya Tatu kuanzia tar 05/07/2021- 03/09/2021=Tshs 155,000] laki moja na elfu hamsini na tano )
- Awamu ya Nne kuanzia20/09/2021-30/11/2020 =Tshs 107,000 ( laki moja na elfu saba tu)

NB**. Ikiwezekana unaweza kulipa michango yote ya chakula kwa awamu moja ili kuepuka usumbufu(NMB-71110026279 Lucas Malia Girls Secondary School)**

**4.0 Angalizo Kwa Mzazi**

- Shule inafuata mihula inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, hivyo inakuwa ni mihula mirefu miwili na mifupi miwili kwa mwaka. Mzazi/mlezi unaombwa kutoa ushirikiano wako kuhakikisha mtoto anawasili kwa wakati shuleni, vinginevyo sheria itachukua mkondo wake.

- Mawasiliano yoyote kati ya mwanafunzi na mzazi/mlezi yafanyike kupitia mkuu wa shule, Makamu mkuu wa shule na ofisi ya malezi. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi awapo shuleni.
- Aidha unashauriwa kutomruhusu mwanao kumiliki simu kipindi hiki ambacho umri wake unampa shida kuyatawala mazingira ya utandawazi.
- Mzazi/mlezi unashauriwa kutompa mtoto fedha nyingi ambazo zitamfanya apoteze utulivu wa maisha ya shule na kuvunja sheria za shule.
- Siku ya kuwatembelea wanafunzi ni jumamosi na jumapili ya mwisho wa mwezi tu, muda ni kuanzia saa nne asubuhi hadi saa kumi na moja jioni.
- Shule ina utaratibu wa kushughulikia usafiri kwa wanafunzi wanaotoka mbali kipindi shule inapofunga. Hivyo mzazi/mlezi utapewa taarifa kabla ya shule kufunga.
- Mzazi hakikisha unapima afya ya mwanao kwa uaminifu ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo
- Iwapo mwanao ana ugonjwa unaomsumbua mara kwa mara, tafadhali aje na vyeti pamoja na dawa anazotumia na akabidhi kwa muuguzi wa shule. Hii itarahisishia shule kumhudumia. Usipofanya hivyo shule itashindwa kumhudumia. Usifiche ugonjwa, utapokelewa tu, kupata elimu ni haki yako.
- Mwanafunzi anaruhusiwa kuleta pasi ya mkaa kwa ajili ya kunyooshea nguo zake. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na kutumia pasi ya umeme ama kifaa chochote kinachotumia umeme. Akibainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwemo kusimamishwa shule.
- Shule itakapofungwa, likizo zote mwanafunzi atatokea shuleni moja kwa moja kwenda kwa mzazi wake (nyumbani kwao) na shule itakapofungua atatokea nyumbani kwao (kwa mzazi/mlezi) moja kwa moja kuja shuleni. Atakayekiuka utaratibu huu atarudishwa nyumbani kwa gharama zake.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na kumiliki simu au kifaa chochote kinachohusiana na simu, hata kama anatoka mbali. AKIJA NAVYO ATAFUKUZWA SHULE (ATAFUTWA MASOMO MARA MOJA)

**N.B**: Tafadhari mshauri mwanao azingatie/afuate maelekezo yote aliyopewa! Akipatikana na kosa litakalimsababisha arudishwe nyumbani, atajigharamia nauli ya kwenda na kurudi.

**5.0 Sheria za shule**

- Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu na kuwatii wakubwa wote
- Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu wanafunzi wanzake, kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa chakula, ofisi za shule, jiko la shule n.k
- Yakupasa kuweka shule, eneo lake na wewe binafsi katika hali ya usafi wakati wote
- Mwanafunzi aheshimu kengele, awahi katika mikusanyiko na kila mahali anapotakiwa
- Mwanafunzi anapaswa kuwa kimya darasani wakati wa kujisomea.
- Mwanafunzi anapopata shida kubwa kama kufiwa au kuugua ruhusa ya kwenda nje ya shule itatolewa na mkuu wa shule au makamu wake
- Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi au viambatanisho vyake kama charger, line, earphones’’ pamoja na redio
- Mwanafunzi haruhusiwi kupiga simu popote bila kibali cha uongozi wa shule, ili kuepuka upelekaji wa taarifa zisizo sahihi kwa wazazi. Mawasiliano yote yatafanywa kupitia ofisi ya makamu mkuu wa shule na ofisi ya malezi tu.
- Wanafunzi hawaruhusiwi kuja au kuletewa chakula cha aina yoyote toka nyumbani
- Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mazungumzo na ndugu/jamaa yake msikitini, kanisani au hospitalini. Kama ndugu/jamaa huyo ana maagizo afike ofisini aonane na uongozi wa shule
- Mwanafunzi haruhusiwi kwenda katika nyumba za walimu au wafanyakazi wengine bila ruhusa maalum.
- Mafuta yenye harufu kali, perfume/spray, poda, rangi za kucha na midomo, wanja, curl,nywele za bandia, mapambo kama bangili, heleni, mikufu n.k. havitakiwi kabisa shuleni.
- Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa,Wimbo wa Taifa, Wimbo wa shule, wimbo wa Tanzania Tanzania Nakupenda kwa Moyo Wote na Tazama Ramani (kila mwanafunzi anatakiwa ajue kuimba nyimbo hizi

- Mwanafunzi haruhusiwi kukaa bwenini wakati wa vipindi au wakati wa kazi, (mwanafunzi mgonjwa anapaswa kupumzika katika chumba maalumu cha wagonjwa).
- Mwanafunzi haruhusiwi kuolewa,
- Mwanafunzi **haruhusiwi kusuka nywele**, wanafunzi wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni, urefu unaowezesha kijiti cha kiberiti kuonekana. Haruhusiwi kunyoa kipara au mitindo mingine kama kiduku, kijoti, kiseven n.k
- Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini/dhehebu awapo shuleni
- Ni marufuku kumruhusu mgeni kufika katika eneo la mabwenini
- Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mtu ambaye si mwanajumuiya wa shule hii isipokuwa kwa kusalimia
- Mzazi/mlezi aliyeandikishwa shule ndiye anaruhusiwa kumwombea ruhusa mwanafunzi kama kuna tatizo. Pia ndiye atakayekuja shuleni pindi atakapohitajika kufanya hivyo
- Wakati wa kufunga shule wanafunzi wote wataondoka kwa pamoja kwa usafiri utakaoratibiwa na shule. Hakuna ruhursa yoyote itakayotolewa mapema kabla ya siku rasmi ya kufunga shule
- Kama mwanafunzi atapatikana na kosa la kinidhamu, mzazi au mlezi ndiye atakayetakiwa kufika shuleni na si mtu mwingine yeyote kama babu, bibi, mjomba, shangazi, kaka n.k.
- Mwanafunzi haruhusiwi kupiga au kupigana na mtu yeyote awapo shuleni
- Mwanafunzi haruhusiwe kutumia lugha chafu.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- Mwanafunzi haruhusiwi kuanzisha, kushawishi na kushiriki mgomo.

**5.1 Adhabu**

Mwanafunzi anaweza kusimamishwa na hatimaye kufukuzwa shule endapo atatenda moja au zaidi ya makosa yafuatayo;

- Wizi wa aina yoyote
- Uasherati, na vitendo vyote vya kujamiana au kuleta hisia za kujamiana.
- Uvutaji bangi, sigara au ulevi wa aina yoyote (Pombe au madawa ya kulevya).
- Kupiga au kupigana na mwanafunzi, wafanyakazi au watu wengine au kusababisha ugomvi.
- Makosa ya jinai.
- Kuolewa
- Kutoa mimba au kusababisha kutoa mimba.
- Kugoma au kuchochea mgomo, kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa wanafunzi na wafanyakazi wote.
- Kukataa adhabu iliyotolewa na uongozi wa shule au mwalimu kwa makusudi
- Kukutwa na simu ya mkononi shuleni.
- Kuleta/kuletewa chakula shuleni toka nyumbani na kuja nacho mabwenini.
- Utoro wa kudumu (Zaidi ya siku 90)
- Kuhujumu au kuharibu mali za shule au mali za watu kwa makusudi.
- Kutumia lugha ya matusi kwa wanafunzi, wafanyakazi au watu wengine.
- Kuandika kwenye kuta za shule; kuta za madarasa, ofisi, mabweni, maabara
- Kufanya udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani kama kuibia kwa mwanafunzi mwenzake, kuingia chumba cha mtihani na karatasi, nguo au vitambaa vilivyo na maandishi n.k.

**Kumbuka** Shule ya Sekondari ya Wasichana Lucas Malia ni shule maalumu, hivyo basi binti yako anatakiwa afaulu zaidi ya alama 30% mtihani wake wa mwisho wa mwaka wa masomo, chini ya alama hizo atatakiwa kurudishwa katika shule yake kata alikotokea.

**KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA *KWANZA* KWA MWAKA 2020**

**Mimi** ……………………………………………………… nakutaarifu kuwa nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari ya Wasichana **LUCAS MALIA**. **NIMEKUBALI/NIMEKATAA** nafasi hii baada ya kusoma na kuelewa yaliyoandikwa katika fomu na barua ya kujiunga.

Ninaahidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu kuwa nikishafika shuleni, nitazingatia kanuni, sheria na taratibu zote za shule kwa kipindi chote cha mimi kuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Lucas Malia. Na nimeelewa kanuni na taratibu zote za shule na sitajihusisha na vitendo vya uvunjaji wa amani shuleni, kushiriki kufanya fujo, vurugu, migomo, kuvuta bangi na matumizi ya madawa ya kulevya pamoja na makosa ya jinai.

Nitatumia juhudi na maarifa katika kujiendeleza kwa manufaa yangu na Taifa kwa ujumla.

**Jina la mwanafunzi** ……………………………… **Sahihi** ….….……….… **Tarehe**……….

**Jina la Mzazi/Mlezi** ……………………………… **Sahihi** ….….……….… **Tarehe**……….

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING**

LUCAS MALIA GIRLS SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 51,
**RUANGWA.**
DATE……………………

***REF. No. ………………………………***
**To the Medical Officer**
………………………………………………………………….….
…………………………………………………………………….**.**

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO …….…………………………**

Please examine the above named pupil and give us the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school students.

1. Blood……………………………………………………………………………
2. Stool ……………………………………………………………………………….
3. T.B.Test ……………………………………………………………………..
4. Syphilis Test ………………………………………………………………………
5. Urine Examination ……………………………………………………………..
6. Eye Test ……………………………………………………………………..
7. Chest Test …………………………………………………………………………
8. Ears Test ………………………………………………………………………….
9. Spleen …………………………………………………………………………….
10. Abdomen ……………………………………………………………………….
11. Pregnancy……………………………………………………………………….

ANY ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairment, infection, family diseases etc.
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
…………
I certify that, the above pupil is suitable/unsuitable for secondary school students. If unsuitable give reasons: ……………….…………………………………………………………...
……………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………….

**Name of Medical Officer:** …………………………………  Signature ………………………

Date: ……………………………………… Official stamp ………………………………

**FOMU NAMBA 2.**

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Mkoa…………………..……
2. Wilaya …………………
3. Tarafa …………………………………………….
4. Kata …………………………………………
5. Mtaa/Kijiji ……………………………………………
6. Jina la Mtendaji wa Kijiji/Mtaa………………………………..Saini………………….

   Tarehe……………Mhuri……………………………. Simu…………………...

5. Michezo anayopendelea

| **Na.** | **Jina la Mchezo** |
|---|---|
| 1. | |
| 2. | |
| 3. | |
| 4. | |
| 5. | |

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pamoja na kuwa na bidii ya masomo.

**NB**: Pamoja na fomu hizi ambatanisha na nakala ya  cheti chako cha kuzaliwa

**Jina la Mwanafunzi …………………………..Sahihi ………………… Tarehe ……………**

**FOMU NAMBA 3.**

**TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………
2. Kazi …………….……………………………………………………………………….
3. Anuani …………………………… Namba ya simu ……………………………….
4. Mkoa………………………Wilaya……………………….. Tarafa ………….………
5. Kata ………………………………………Mtaa/Kijiji ………………………………

6. Anuani kamili ya nyumbani ambako  mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo

| Na. | JINA | UHUSIANO | ANAPOISHI | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |
| 6. | | | | |

Mimi Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………………… ninaahidi kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Lucas Malia katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa shuleni.

Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sheria, kanuni  na taratibu za shule. Pia nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya.

**Jina la Mzazi/Mlezi …………………………Sahihi ………………Tarehe ………………..**